## MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA, 2022) KWA MKOA WA SHINYANGA

### Umetolewa: (02/09/2022)

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba - Disemba, 2022; athari na ushauri kwa sekta mbalimbali katika mkoa wa Shinyanga na wilaya zake:

(I) Ngazi ya Mkoa

(a) (b)




Kielelezo 1: (a) Mwelekeo wa msimu wa Vuli, 2022 kwa mkoa wa Shinyanga. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Vuli katika sehemu mbalimbali za mkoa wa Shinyanga. **Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Oktoba hadi Disemba, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

**Dondoo**

- *Kwa ujumla mvua za Chini ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mkoa wa Shinyanga.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya nne ya Oktoba, 2022.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha Januari, 2023.*
- *Vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi vinatarajiwa katika msimu huu wa Vuli.*

**Mvua za msimu wa Vuli, 2022**

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya wilaya za mkoa wa Shinyanga. Msimu unatarajiwa kuanza kwa kusuasua na kuambatana na vipindi virefu vya ukavu.

***Angalizo:***

*Ingawa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo machache.*

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA, 2022) KWA WILAYA YA SHINYANGA
### Umetolewa: 02 /09/2022

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Shinyanga.




Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba, 2022) kwa wilaya ya Shinyanga.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Shinyanga.*
- *Mvua zitaanza wiki ya nne ya Oktoba, 2022 na zinatarajiwa kuanza kwa kusuasua kutokana na kuwepo vipindi virefu vya ukavu.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha Januari, 2023.*
- *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

### Mvua za msimu wa Vuli, 2022 kwa wilaya ya Shinyanga

**Zitaanza:** Wiki ya nne ya Oktoba, 2022.

**Zitaisha:** Januari, 2023.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba-Disemba kwa wilaya ya Shinyanga ni kati ya milimita 250 hadi 320.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2022.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

**Matokeo**

- Upungufu wa unyevunyevu katika udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao.
- Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

**Ushauri**

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.
- Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.

(II) Ngazi ya Wilaya

# MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA, 2022) KWA WILAYA YA KISHAPU, SHINYANGA

## Umetolewa: 02/09/2022

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kishapu, Shinyanga.




Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba, 2022) kwa wilaya ya Kishapu, Shinyanga.

## Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kishapu.*
- *Mvua zitaanza wiki ya nne ya Oktoba, 2022 na zinatarajiwa kuanza kwa kusuasua kutokana na kuwepo vipindi virefu vya ukavu.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha Januari, 2023.*
- *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

## Mvua za msimu wa Vuli, 2022 kwa wilaya ya Kishapu

**Zitaanza:** Wiki ya nne ya Oktoba, 2022.

**Zitaisha:** Januari, 2023.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba-Disemba kwa wilaya ya Kishapu ni kati ya milimita 230 hadi 300.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2022.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

## Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

### Matokeo

- Upungufu wa unyevunyevu katika udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao.
- Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

### Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.
- Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA, 2022) KWA WILAYA YA KAHAMA, SHINYANGA

### Umetolewa: 02 /09/2022

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kahama, Shinyanga.




Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba, 2022) kwa wilaya ya Kahama, Shinyanga.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kahama.*
- *Mvua zitaanza wiki ya nne ya Oktoba, 2022 na zinatarajiwa kuanza kwa kusuasua kutokana na kuwepo vipindi virefu vya ukavu.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha Januari, 2023.*
- *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

### Mvua za msimu wa Vuli, 2022 kwa wilaya ya Kahama

**Zitaanza:** Wiki ya nne ya Oktoba, 2022.

**Zitaisha:** Januari, 2023.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba-Disemba kwa wilaya ya Kahama ni kati ya milimita 290 hadi 340.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2022.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

- Upungufu wa unyevunyevu katika udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao.
- Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

#### Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.
- Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.




*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Morogoro Rd, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3,
S.L.P. 3056, Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8.
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz



**(IMETHIBITISHWA – ISO 90:25, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*105A – 09/19*

Taarifa hii Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania